

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



18 JUNI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE – TAREHE 18 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

445. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA
(VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni kwa kiasi gani Mifuko ya Uwezeshaji Kiuchumi iliyoanzishwa kwa lengo la kuwaondolea Wananchi umaskini na kuwajengea uwezo wa kiuchumi imewanufaisha Wanawake wa Kitanzania waliopo nje ya Mkoa wa Dar es Salaam.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

446. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Daraja lililopo katika Barabara ya Kishinda B limefunikwa na maji na kukatisha Mawasiliano kwa Wananchi wa Kata za Nyaruzumbura, Nyakatuntu, Kakanja, Kikukuru, Mabila na Kitwe:-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja hilo ili kuwarejeshea mawasiliano Wananchi.

447. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Suala la Vitambulisho vyatya ujasiriamali limekuwa ni changamoto hasa kwa Wafanyabiashara wenyewe mitaji midogo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha au kufuta Vitambulisho hivyo.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

448. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini Serikali itaondoa changamoto ya Kukaimu muda mrefu kwa Watumishi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Sekretarieti za Mikoa.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

449. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA (MKINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Tanga – Mabokweni – Maramba – Daluni – Mtoni – Bombo – Magoma hadi Korogwe.



WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

450. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni chombo gani kinasaidia Abiria kupata haki pindi anapopata ajali akiwa safarini.

WIZARA YA MAJI:

- 451. MHESHIMIWA DKT. STEVEN LEMOMO KIRUSWA (LONGIDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Tarafa ya Enduimet pamoja na Vijiji vya Elerai, Tingatinga na Sinya vitaunganishwa na Mradi wa Maji kutoka Mto Simba hadi Longido ambao umepita katika maeneo hayo.

- 452. MHESHIMIWA EDWARD KISAU OLELEKAITA (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa Wananchi wa Jimbo la Kiteto wananaufaika na Miradi ya Maji safi na salama ili waweze kufikia azma ya asilimia 85 na 95 Vijijini na Mijini ifikapo Mwaka 2025.

WIZARA YA NISHATI:

- 453. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

(a) Je, ni Vijiji vingapi vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya vimepata umeme wa REA II, *Densification* na REA III;

(b) Je, ni lini Vijiji vilivyobaki vitapatiwa umeme.

454. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Wananchi wa Makambako watalipwa fidia baada ya maeneo yao kuchukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuzalisha umeme wa upepo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
18 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, ndc
KATIBU WA BUNGE**